## Maswali

1. Mbona Hamani alikasirikia Mordekai?
2. Hamani alipanga kuadhibu Mordekai namna gani?
3. Mordekai alitaka Esta afanye nini?
4. Mbona Esta hakutaka kwenda kumuona?
5. Kwa siku 3 Esta na Wayahudi walifanya nini Shushani?
6. Mfalme alifanya nini Esta alipoenda kumwona?
7. Hamani angefanya nini kuzawadisha Mordekai kwa kumwokoa Mfalme?
8. Esta aliuliza Mfalme nini walipokuwa kwa karamu?
9. Hamani aliadhibiwa namna gani?
10. Esta na Mordekai waliweka amri gani?

## Majibu

1. Hamani alikasirikia Mordekai kwa sababu hakumwinamia.
2. Hamani alipanga kuangamiza Wayahudi wote siku ya 13 mwezi wa 12.
3. Kuenda kuona Mfalme na kumuuliza aokoe Wayahudi.
4. Mtu yeyote akienda kuona Mfalme bila kukaribishwa angeuawa.
5. Esta na Wayahudi wa Shushani walifunga na kuomba kwa siku 3.
6. Mfalme alimnyoshea Esta fimbo yake ya dhahabu.
7. Alimwongoza juu ya farasi wakizunguka mji wote akisema kwamba Mfalme amemfurahia Mordekai.
8. Esta aliuliza Mfalme amwokoe yeye na Wayahudi wote.
9. Hamani alitundikwa juu ya mti alioutengeneza ili amuie Mordekai.
10. Wayahudi wangeuwa maadui wao siku ya 13 mwezi wa 12.

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM

**Awamu ya 2 Mwaka wa 2**

# 87 Esta na Wayahudi wanaokolewa

## Kwa Biblia

Esta mlango wa 3 mpaka mlango wa 8

## Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu hulinda watu wake. Mungu hutumia matokeo ya dunia kutimiza kuzudi zake

## Somo

Hamani alikuwa mkubwa wa wakuu wa nyumba ya kifalme ya Mfalme Ahasuero. Katika Ufalme wa Uajemi, Hamani alikuwa mtu wa pili kwa madaraka. Ilikuwa desturi ya kila mtu kuinamia mtu mkuu. Hamani alikuwa mtu wa majivuno. Alitaka kila mtu amwinamie.

Mordekai alikuwa myahudi. Mordekai alikuwa mtu wa maana katika mji wa Shushani. Lakini Mordekai hakuinamia Hamani. Mungu alikuwa ameamrisha Wayahudi kumwinamia na kuabudu yeye tu. Hamani alikasirika sana kuona kwamba Mordekai hamwinamii. Hamani aliamua kuadhibu Mordekai. Hamani alijua kwamba Mordekai alikuwa Myahudi. Alipanga kuangamiza Wayahudi wote. Hamani alikuwa na majivuno tena mkatili. Mordekai alimkasirisha Hamani sana. Hamani hakutaka kuua mtu mmoja, alitaka kuangamiza taifa nzima. Hamani akapanga kuangamiza Wayahudi wote kwa sababu Mordekai hakumwinamia.

Hamani alipanga kwa kisiri. Alichagua kuangamiza Wayahudi siku ya 13 mwezi wa 12. Hamani alitaka Mfalme aweke sheria ya kuwaangamiza Wayahudi.

Hamani alikuwa mchanja. Hakuambia Mfalme juu ya adui wake Mordekai. Hamani aliambia Mfalme kwamba Wayahudi huweka na kutii amri zao. Alimwambia kwamba niwasumbuvu katika taifa. Aliambia Mfalme aweke sheria ya kuwaangamiza Wayahudi wote. Aliahidi kumpa Mfalme talanta 10,000 za fedha ikiwa ataweka hiyo sheria.

Mfalme alikubali kuweka sheria. Alipea Hamani pete yake. Hamani aliandika hiyo sheria na kuweka muhuri wa pete ya Mfalme. Sheria ilisema kwamba, lazima Wayahudi wauawe siku ya 13 mwezi wa12.

Sheria iliandikwa na kuwekwa muhuri. Iliandikwa na kutafsiriwa kwa kila lugha ya eneo lote la huo ufalme. Sheria hiyo ilipelekwa na wajumbe wa Mfalme. Ilipelekwa kila mahali kwa ufalme wote. Sheria ilisema kwamba kila Myahudi auawe siku ya 13 mwezi wa 12.

Wayahudi wa Shushani walisikia habari ya hiyo sheria. Waligadhabika sana. Mordekai naye alisikia habari ya hiyo sheria. Alipelekea Esta nakala ya hiyo sheria. Mordekai aliambia Esta aende kwa Mfalme. Alimwambia aambie Mfalme aokoe Wayahudi, watu wake. Esta hakuwa ameambia mtu yeyote kwamba yeye ni Myahudi. Mfalme hakujua kwamba Esta ni Myahudi.

Kulikuwa na sheria kwamba mtu yeyote hangeenda kuona Mfalme kama hajakaribishwa. Kama mtu angeenda kuona Mfalme na hajakaribishwa, angeuawa. Wangepona tu, ikiwa Mfalme angewanyoshea fimbo yake ya dhahabu. Mfalme hakukuwa amemkaribisha Esta kumwona kwa muda wa mwezi hivi. Esta alitumia Mordekai ujumbe. Hangeweza kuenda kuona Mfalme kama hajamkarbisha.

Mordekai alijua kwamba Esta ndiye alikuwa mtu wa pekee atakaye okoa Wayahudi. Esta lazima ahatarishe maisha yake na aokoe Wayahudi, watu wake. Mordekai alitumia Esta ujumbe akisema, “Usifikiri kwamba wewe utahepa kifo. Ukikataa kusaidia Wayahudi, tutasaidiwa kwa njia nyingine. Lakini wewe utaadhibiwa kwa kutosaidia watu wako. Umekuwa Malkia ili usaidie Wayahudi.”

Esta alikubali kusaidia Wayahudi. Alisema, “Nitaenda kumuona Mfalme hata kama ni kufa, wacha nikufe.” Esta pamoja na Wayahudi wote waliokuwa Shushani walifunga na kuomba kwa siku tatu. Halafu Esta alienda kumuona Mfalme.

Mfalme Ahasuero alishutuka kumuona Esta. Alimnyoshea fimbo yake ya dhahabu. Uhai wake uliokolewa! Siku hiyo Esta alikaribisha Mfalme pamoja na Hamani kwa karamu yake. Tena kwa siku ya pili akawakaribisha kwa karamu nyingine. Esta aliambia Mfalme kwamba alikuwa na jambo la mhimu la kumwomba. Alisema atamwambia hilo ombi kesho yake kwa karamu nyingine.

Hamani alijivuna kwa sababu alikuwa amekaribishwa kwa karamu ya Malkia. Alipokuwa akienda nyumbani aliona Mordekai. Mordekai hakumwinamia. Hamani alikasirika sana. Akaamua kwamba atamuua Mordekai. Hamani alitengeneza mti mrefu atakaotundika Mordekai kesho yake.

Usiku huo Mfalme hakuweza kulala. Aliita mtumishi aje amsomee taarifa za kifalme zote. Alisoma mahali penye Mordekai alipata kwamba kulikuwa na mpango wa kua Mfalme. Aliuliza kama amewahi kumpa Mordekai zawadi yoyote kwa kumwokoa. Ilipatikana kwamba hajawahi kumpa zawadi yoyote.

Asubuhi iliyofuata, Hamani alikuja kwa Mfalme. Alikuja kuuliza Mfalme ili amtundika Mordekai kwa huo mti mrefu. Kabla ya kusema hayo, Mfalme alimtuma amzawadishe Mordekai. Hamani alimtembeza Mordekai kwa mji wote juu ya farasi. Hamani alipaza sauti akisema, “Huyu ni mtu aliyefurahisha Mfalme.” Hamani alikasirika na kuudhika sana.

Mfalme na Hamani walienda kwa karamu ya Esta. Esta aliuliza Mfalme aokoe uhai wake. Alimuuliza aokoe pia watu wake, Wayahudi. Mfalme alikasirika sana na kumuuliza, “Ni nani huyu anataka kufanya kitendo kibaya hiki.” Malkia Esta alijibu, “Adui wetu ni huyu mtu muovu, Hamani.” Mfalme alikasirika sana. Hamani alitolewa nje. Alitundikwa kwa mti wenye alikuwa ametengeneza amweke Mordekai ili afe.

Mfalme alifanya Mordekai awe mkubwa wa wakuu badala ya Hamani. Sheria haingeweza kubadilishwa. Kwa hivyo Mfalme akaweka amri kwamba Wayahudi waue adui wao siku ya 13 mwezi wa 12. Sheria hiyo ilisambaza kwa Ufalme wote. Hivo Wayahudi waliokolewa. Mungu alitumia maisha ya hawa watu kuokoa Wayahudi.